

Wasemavyo wadau Kuhusu kupima

Ningependa (Ubora wa elimu) uonekane kwa matokeo baada ya kumaliza shule, sihitaji kusikia amefaulu kwa alama ngapi ili amejengewa uwezo gani kichwani



Dr Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia, na Ufundi Tanzania.
(Mwananchi, 1 January 2016)

Kupima kwa ajili ya kujifunza inakusudisha kuboresha ujifunzaji kwa kurekebisha yanayofundishwa pamoja na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji



Mwalimu, Shule ya Msingi

Kupima kwa ajili ya kujifunza inassidila kuwashirikisha wanafunzi kwa lengo la kuboresha ujifunzaji



Mwalimu, Shule ya Msingi

Chuo Kikuu cha Aga Khan,
Taasisi ya Kuendeleza Elimu,
Afrika Mashariki



Timu ya KUKUA



THE AGA KHAN UNIVERSITY



Tshwane University of Technology
UNIVERSITY OF TECHNOLOGY



Centre for International Teacher Education
E-S-R-C
ECONOMIC
AND
SOCIAL
RESEARCH
COUNCIL
From the United Kingdom



Research partly supported by the ESRC and DFID



UNIVERSITY OF
OXFORD

Washirika wa KUKUA nchini Tanzania:

Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi - Ofisi ya Rais -
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) - Ofisi za Elimu
za mikoa na wilaya • Vyuo vya ualimu • Shule za msingi.

Kwa taarifa zaidi, wasiliana na;

Profesa Anjum Halai

Chuo Kikuu cha Aga Khan, Taasisi ya Kuendeleza Elimu, Afrika Mashariki.

utafiti.kukua@aku.edu

<http://oucea.education.ox.ac.uk/reseach/recent-reseach-projects/assessment-for-learning-in-africa-afla/>

USHIRIKIANO WA KIUTAFITI

Kupima kwa ajili ya Kujifunza, Afrika (KUKUA)

KUPIMA kwa ajili ya KUJIFUNZA AFRIKA (KUKUA)



Kipaumbele cha mradi wa utafiti wa KUKUA unaofanyika nchini Tanzania na Afrika Kusini, ni kuinua viwango vya stadi za hisabati za watoto mashulenii. Utafiti utafanya kazi na walimu kuinua viwango vya ufundishaji hisabati katika shule za msingi kujitia upimaji wa darasani wenye ufanisi.

Kujitia mradi huu tunatarajia kujifunza mbinu za kufundishia na jinsi walimu wanavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuongeza stadi zao za hisabati. Jinsi walimu wanavyoweza kuinua viwango vyao vya ufundishaji kwa utaratibu wa kupima ujifunzaji madarasanii. Na ni kwa jinsi gani walimu wanaweweza kuwasaidia wanafunzi kujua hatua waliyofikia katika kujifunza.

KUPIMA KWA AJILI YA KUJIFUNZA NI NINI?

- Mwalimu kufahamu kwa kina yapi yanayolewaka na yapi hayaeleweki na wanafunzi wake.
 - Mwalimu kupanga ufundishaji wake kulingana na ufahamu, uwezo na udhaifu wa wanafunzi wake.
 - Mwalimu kuufanya mazingira ya darasa yafae kwa ufundishaji na unoasaidia ujifunzaji wa watoto.
 - Mwalimu kuwashirikisha wanafunzi wake kwa kutumia upimaji-rika na upimaji-binafsi kwenye hisabati
 - Mwalimu kuboresha alama za wanafunzi kwa kutumia mbinu za darasani zenyenye ufanisi.



NINI MATOKEO YA UTAFITI HUU?

Matokeo ya utafiti huu yanatarajia kutufundisha mbinu mpya na za kusisimua zaidi za kupima viwango vya hisabati. Zana za kupimia zitakazotumiwa na walimu na zile zitakazotumiwa na wanafunzi wa shule za msingi kujifunza. Alina za maelezo na warsha kwa ajili ya walimu na taarifa au ripoti za mara kwa mara kwa ajili ya wadau wote.



WADAU NI NANI?

Wadau wa mradi huu ni wanafunzi na walimu wote wa shule za msingi, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wazazi na walezi, wizara na idara za Serikali, mashirika ya kitaifa na klimataifa, taasisi zinazohusika na upimaji wa elimu na wanazuoni na watafiti kwa ujumla.



NINI MCHANGO WAKO?

Kufanikisha mradi huu unaweza kutuandikia maoni yako, kutushirikisha dhana za kufundishia unazotumia darasani. Unaweza ukaamsha shauk ya kujifunza hisabati darasani kwako au ukahudhuria warsha zetu. Unaweza pia ukajaribu mbinu mpya za ufundishaji na kuwaambia wengine habari za mradi huu.

